# KUZUIA KASWENDE NA UTUNZAJI:
## Vidokezo kwa Mashirika ya Jamii

Hatua unazoweza kuchukua kama mtoa huduma ili kusaidia wateja kuzuia kaswende na utunzaji

**Kama mtoa huduma, wewe ni mshirika muhimu katika juhudi za Kanada za kupunguza viwango vya maambukizi ya ugonjwa wa kaswende. Kupitia uhusiano ulioimarishwa pamoja na watu muhimu katika jamii zako, unaweza kuendelea kusaidia watu kuona mazungumzo kuhusu afya ya ngono kuwa ya kawaida na yasiyo ya aibu na uwe mtu wa kwanza ambaye anaweza kufikiwa na wateja wanaoweza kuhisi vibaya kufikia mfumo wa huduma ya afya.**

# Vidokezo vya Kujadili na Wateja Kuhusu Kuzuia Kaswende na Utunzaji

## Jifunze

### Jifunze kuhusu kuzuia, kupima na matibabu ya kaswende

- Rejelea vyanzo vya kuaminika, kama vile nyenzo zilizochapishwa na serikali au watu wenye maarifa ya afya ya ngono, ili kustarehe zaidi katika kujadili kuhusu kuzuia kaswende na utunzaji
- Tembelea viungo vifuatavyo ili upate nyenzo za ziada ili uweze kujifunza zaidi :
  - Kaswende, Shirika la Afya ya Umma la Kanada (Public Health Agency of Canada, PHAC) : https://www.canada.ca/syphilis
  - Nyenzo za kaswende, CATIE: https://www.catie.ca/syphilis-resources

## Wasiliana

### Shiriki habari muhimu na ujiandae kujibu maswali kuhusu kaswende

**Umuhimu**

- Mtu asipotibiwa kaswende, jambo hilo linaweza kusababisha matatizo makubwa ya kiafya, na kuathiri viungo na mifumo mingi ikijumuisha ubongo, macho, moyo, neva na mifupa
- Mtu asipotibiwa kaswende akiwa mjamzito, jambo hilo linaweza kusababisha kuharibika kwa mimba au mtoto kuzaliwa akiwa amekufa, au kufanya mtoto azaliwe akiwa na kaswende
- Ingawa watu wengi hawafikirii kuwa wako hatarini, mtu yeyote ambaye anashiriki tendo la ngono anaweza kupata kaswende
- Visa vya ugonjwa wa kaswende vinaongezeka nchini Kanada; mnamo 2022 kulikuwa na visa 13,953 vilivyoripotiwa vya kaswende ya kuambukiza na visa 117 vya watu waliozaliwa wakiwa na kaswende



Canada

**Uambukizaji**

- Kaswende ni ugonjwa wa zinaa ambao mtu anaweza kuambukizwa kupitia kugusana moja kwa moja na kidonda cha kuambukiza wakati wa ngono ya uke, mkundu, au mdomo
- Kaswende pia inaweza kuambukizwa watoto wakati wa ujauzito kupitia plasenta, au wakati wa kuzaliwa kwa kugusana moja kwa moja na kidonda cha kuambukiza
- Kaswende huambukiza zaidi katika hatua za mwanzo wakati ambapo huenda watu wasione dalili zozote

**Kupima**[1]

- Kwa kawaida kaswende hupimwa kupitia sampuli za damu; usufi pia unaweza kuchukuliwa kwa vidonda au upele wowote
- Kupimwa kaswende kunapendekezwa kwa watu wote wanaofanya ngono na mwenzi mpya au wapenzi wengi, na/au mtu akiomba kupimwa
- Kupimwa kaswende kunapendekezwa kila baada ya miezi 3 hadi 6 kwa watu walio na wapenzi wengi wa ngono
- Upimaji wa jumla unapendekezwa kwa wanawake wajawazito katika miezi mitatu ya kwanza au katika ziara ya kwanza ya ujauzito, na upimaji mwingine unapendekezwa katika miezi mitatu ya mwisho na wakati wa maumivu ya kuzaa kwa watu walio katika hatari kubwa

**Matibabu**

- Ugonjwa wa kaswende unaweza kutibiwa na kuponywa kwa dawa za viua vijasumu, ambazo kwa kawaida hutolewa kwa kudungwa sindano, na zinaweza kusaidia kuzuia kuambukiza washirika wa ngono
- Matibabu ya kaswende wakati wa ujauzito ni salama na yanaweza kuzuia kaswende kupitishwa kwa watoto wanaokua

**Ufuatiliaji**

- Ufuatiliaji wa mara kwa mara kupitia kupimwa baada ya matibabu ni muhimu ili kuthibitisha kuwa kaswende imeponywa, na ni fursa ya kupokea taarifa muhimu kuhusu afya ya ngono na uzazi ili kuwa na afya katika siku zijazo

**Taarifa**

- Matokeo ya wale ambao wamepatikana na ugonjwa huo baada ya kupimwa yanaripotiwa kwa vitengo vya afya ya umma ili kusaidia kufuatilia afya ya jamii nzima
- Ni mteja pekee, mhudumu wao wa afya na muuguzi wa afya ya umma ambao watajua kuwa ana maambukizi
- Muuguzi wa afya ya umma anaweza kujitolea kumsaidia mteja kuwaarifu washirika wake wa ngono wa sasa na wa zamani kwamba wanahitaji kupimwa

## Msaada

### Husaidia wateja kuabiri huduma za afya ya ngono na usaidizi mwingine wa kijamii

- Tembelea viungo vifuatavyo ili upate nyenzo za ziada zinazoweza kukusaidia kusaidia wateja wanaotumia huduma za afya ya ngono na usaidizi mwingine wa kijamii:
  - Kitafuta huduma, CATIE: https://whereto.catie.ca/
  - Huduma na usaidizi ulio karibu nawe, NWAC: https://stbbi.nwac.ca/services-and-supports-near-you/

[1]Maelezo zaidi, angalia Miongozo ya STBBI ili kupata Wataalamu wa Afya: Mwongozo wa kaswende: Uchunguzi na upimaji wa kimatibabu - Canada.ca. Mapendekezo hayachukui nafasi ya mahitaji ya sheria ya mkoa/eneo, udhibiti, sera na utendaji au miongozo ya kitaalamu ambayo inasimamia utendaji wa wataalamu wa afya katika maeneo yao husika, ambayo mapendekezo yake yanaweza kutofautiana kutokana na magonjwa ya eneo au muktadha.

©Mfalme Mkuu katika Haki ya Kanada, kama ilivyowakilishwa na Waziri wa Afya, 2024 Pub: 230894 | Cat: H14-581/2024Swa-PDF // H14-581/2024Swa (Print) |
ISBN: 978-0-660-70887-4 (PDF) / 978-0-660-70888-1 (Print)



Canada